Kwa Nini Mungu Anaruhusu Mateso?

na

Ellis P. Forsman

Kwa Nini Mungu Anaruhusu Mateso?

na

Ellis P. Forsman

Oktoba 17, 2011

Kwa Nini Mungu Anaruhusu Mateso?

2 Wakor. 5:1-5

Kuna swali lililozeeka linalofafana na chozi la kwanza, na lililo mapema kitu kilichozeeka.

"Kwa nini Mungu anaruhusu mateso, uzuni, kuumwa moyo, na kifo, hata kati ya watoto wake?"

Swali hili liliulizwa na Ayubu, na pia limeulizwa na karibia kila mtu ambaye amewahi kutembea katika uso wa nchi na anayeamuamini Mungu.

Limewai pia kuulizwa na Wakristo ambao wamepitia ajali, wao binafsi.

Kusudi la somo hili si kutafuta CHANZO au SABABU ya mateso, bali kuelewa kwa uzuri:

- Kwa nini Mungu anairuhusu.
- Kwa nini Wakristo wanapaswa kushangilia hata wakiwa katikati ya majaribu!

Sababu ya kwanza ni...

Mateso yanaifanya dunia hii isiwe na mvuto sana

Biblia inatuambia kuwa sisi ni "wapitaji" na "wasafiri".

Zingatia vifungu vifuatavyo:

- 1 Petr. 2:11, *"Wapenzi nawasihi kama wapitaji na wasafiri, ziepukeni tama za mwili zipinganazo na roho."*
- Waeb. 13:14, *"Maana hapa hatuna mji udumuo, bali twautafuta ule ujao."*
- 2 Wakor. 5:1, "*Kwa maana twajua ya kuwa nyumba ya maskani yetu iliyo ya dunia hii ikiharibiwa tunalo jingo litokalo kwa Mungu, nyumba isiyofanywa kwa mikono, iliyo ya milele mbinguni."*

Kama kusingekuwa na mateso...

- Hakuna mtu ambaye angependa kuacha dunia hii ya muda mfupi.

- Hakuna mtu ambaye angependa mji wa “milele” na kwa hiyo wajiandae kwa ajili yake.

Kama mapendekezo yao yalikuwa katika mambo ya dunia hii kutakuwa na mapendekezo madogo kwa mambo ya Mungu.

Lakini mambo yote ya maisha haya yamepangiliwa kwamba dunia hivi karibuni inapoteza mvuto wake. Vijana wengi leo wanataka kuishi milele, lakini wakati mtu anapofikia umri wa miaka “ishirini na arobaini” anaanza kutamani kitu kingine bora.

Mateso yanaweza kutuletea vilivyo bora

Mtu aliyeumia vibaya anaweza kuona...

- Msaada wa hapo hapo na rafiki.
- Katika maandalizi ya chakula.
- Msaada wa kifedha.

Tunaona hii utokea mara nyingi...

- Wakati wa majanga ya asili
- Wakati mtu anapoteza nyumba yake kutokana na janga la moto.
- Katika wakati maradhi.

Hii inaweza kuwa sababu ya wakristo wa kwanza kufurahia majaribu yao

Walitambua kwamba matatizo yanaweza kujenga tabia.

Kama Paulo alivyoandika katika Warumi 5:3-4, *“Wala si hivyo tu, ila na mfurahi katika dhiki pia; mkijua ya kuwa dhiki, kazi yake ni kuleta saburi; na kazi ya saburi ni uthabiti wa moyo; na kazi ya uthabiti wa moyo ni tumaini.”*

Mateso yanatoa muda wa kuwanyamazisha maadui wa Mungu.

Kumbuka historia ya Ayubu? Shetani alitaka kuhakikisha kuwa Mungu anakosa juu ya Ayubu, kwamba alimtumikia Mungu kwa sababu tu Mungu ali mbariki. Lakini uvumilivu wa Ayubu chini ya mateso yalinyamazisha shetani!

Vile vile, Mungu anapenda tuwanyamazishe “watu wajinga”.

1 Petr. 2: 15, *“Kwa sababu ndiyo mapenzi ya Mungu, kwamba kwa kutenda mema mzibe vinya vya ujinga vya watu wapumbavu.”*

Watu wajinga wanao dhihaki mafundisho ya Kristo kama ni ujinga.

Watu wajinga wanao sema sisi ni Wakristo kwa sababu tu ya mambo mazuri tunaweza kutoka nje ya ukristo, (tunaweza kuacha).

Jinsi gani? Kwa kuvumilia, au kufanya mema wakati wa mateso.

Ubora wa kuwa mkristo hakika inang'aa kupitia imani tuliyonayo inayotushikilia katika mateso, na katika upendo tunao onyesha kwa wale wanao teseka.

Mateso yanatufanya kuwa bora katika njia nyingi

Mateso yanatufanya tushukuru. Sote tunapokea vitu vizuri vingi katika maisha haya; ni rahisi kwetu kuvipokea kwa shingo upande, badala ya kuvipokea kwa shukurani kwa Mungu.

Mateso yanaweza kutufanya tushukuru zaidi...

- Afya bora.
- Marafiki wazuri na familia yenye upendo.

Mfano mzuri wa jinsi mateso yanaweza kumfanya mtu ashukuru ni Mtume Paulo wakati alipokuwa gerezani.

Wail. 1: 3-8, *"Namshukuru Mungu wangu kila niwakumbukapo , siku zote kila niwaombeapo ninyi nyote nikisema sala zangu kwa furaha, kwa sababu ya ushirika wenu katika kuieneza injili, tangu siku ile ya kwanza hata leo hivi. Nami niliaminilo ndilo hili, ya kwamba yeye aliyeanza kazi njema mioyoni mwenu ataimaliza hata siku ya Kristo Yesu, vile vile kama ilivyo wajibu wangu kufikiri haya juu yenu nyote; kwa sababu ninyi mmo moyoni mwangu; kwa kuwa katika kufungwa kwangu, na katika kazi ya kutetea injili na kuithibitisha, ninyi nyote mmeshirikiana name neema hii. Maana Mungu ni shahidi wangu, jinsi ninavyo waonea shauku ninyi nyote katika moyo wake Kristo Yesu."*

Mateso yanatufanya tumtegemee sana Mungu.

Mara nyingi, tunajifikiria wenyewe kuwa tumejitosheleza. Lakini watu wengi walio na upeo mkubwa katika kazi zao wanakuwambia wamefanya kila wawezalo lakini wameshindwa na pia hawana mikononi mwao, ghafla unakumbuka ni kiasi gani unamtegemea Mungu.

Hakuna wakati mwingine wo wote ambao mtu anaweza kufikiria kwamba tunamtegemea Mungu kwa hewa hii tunayo pumua! Kama Paulo alivyosema:

Matendo. 17:28, *"Kwa maana ndani yaake yeye tunaishi, tunakwenda na kuwa na uhai wetu. Kama vile mmoja wenu mtunga mashairi alivyosema, maana sisi sote tu wazao wake."*

Mateso yanasaidia kututakasa.

Zingatia umuhimu wa vifungu wili...

- 1 Petr. 1:6-7, *"Mnafurahi sana wakati huo, ijapokuwa sasa kwa kitambo kidogo, ikiwa ni lazima mmehuzunishwa kwa majaribu ya namna mbalimbali; ili kwamba kujaribiwa kwa imani yenu, ambayo inathamani kuu kuliko dhahabu ipoteayo, ijapokuwa hiyo hujaribiwa kwa moto; kuonekane kuwa kwenye sifa, na utukufu na heshima, katika kufunuliwa kwake Yesu Kristo."*
- Yakobo 1: 2-5, *"Ndugu zangu hesabuni ya kuwa ni furaha tupu, mkiangukia katika majaribu mbalimbali, mkifahamu ya kuwa kujaribiwa kwa imani yenu huleta saburi, saburi na iwe na kazi kamilifu mpate kuwa wakamilifu na watimilifu bila kupungukiwa na neno. Lakini mtu wa kwenu akipungukiwa na hekima na aombe dua kwa Mungu, awapaye wote, kwa ukarimu wala hakemei; naye atapewa."*

Kueleza ni jinsi gani, zingatia kile ninachokisoma juu ya maneno haya kuhusu mtu ambaye mke wake ali jeruhiwa kwenye ajali:

"Maranyingi nilitafuta maisha yangu wakati wa matukio kama haya ili niweze kukiri kila kushindwa kwangu na majaribu kwa Mungu. Sikutaka dhambi zangu zisimame katiak njia ya Mungu alisikia maombi ya kwa ajili ya mke wangu. Hakika ilikuwa inafaa kuwa mkweli kwa Mungu na kwangu binafsi, sasa mimi ni mtu bora leo kuliko zamani."

Nilikuwa na rafiki yangu maarufu shuleni aliyekuwa na chombo Fulani ambaye alifungiwa baiskeli ya kilema haikuweza kumuwezesha izuie mambo yake binafsi na tabia.

Mateso yanatufanya tuwe na huruma.

Paulo aliandika kuhusu uthamani huu wa mateso katika kanisa kule Koritho, katika waraka wa pili.

2 Wakor. 1: 3-4, *"Na ahimidiwe Mungu Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, Baba wa rehema , Mungu wa faraja yote; atufarijiye katika dhiki zetu zote, ili nasi tupate kuwafariji wale walio katika dhiki za namna zote; kwa faraja hizo tunazo farijiwa na Mungu."*

Inatusaidia kuweza kuwa fariji wengine katika matatizo yao.

Tunaweza kudhani kuwa tunatakiwa kuhuzunika na mtu fulani, lakini mpaka tuwe pale binafsi, hakuna uelewa wa kweli wa moyo wao.

Tukiwa na mateso inatufanya kushirikiana zaidi katika huzuni yao.

Waru. 12:15, *"Furaini na hao wafuraio, lieni na hao waliao."*

Kuwa katika mateso inatufanya tuwahudumie wengine vizuri.

Mateso yanatufundisha namna ya kuomba.

Wote tunaweza kuwa watu waombaji. Tunaomba katika wakati muafaka. Tunaomba kwa ajili ya vitu sahihi. Lakini tukiwa katikati ya mateso tunajifunza namna ya kuomba.

- Kwa undani.
- Kuvumilia.
- Kwa kuugua kusikoweza kutamkwa".

Waru.8:26, *"Kadhalika Roho naye hutusaidia udhaifu wetu kwa maana hatujui kuomba jinsi itupasavyo, lakini Roho mwenyewe hutuombea kwa kuugua kusikoweza kutamkwa."*

Mtu ambaye mke wake alijeruhiwa akasema "nimekuwa mtu wa maombi tangu nilipokuwa Mkristo. Lakini si kwa hivi. "Nimejifunza mengi kuhusu maombi wiki chache zilizopita katika miaka ishirini iliyopita. Maombi yangu yatakuwa tofauti maisha yangu yote.

Hitimisho

Je tunaanza kuona kwa nini Mungu MWENYE HAKI na MWENYE HURUMA anavyo weza kuruhusu mateso, hata kwa walio wema?

Tukiangalia mateso vizuri katika mtazamo wa MWANADAMU, hatutaweza kutambua kwa nini mateso yameruhusiwa.

Lakini kumbuka kile ambacho Mungu alisema kupitia nabii Isaya:

Isay. 55: 8-9, *"Maana mawazo yangu si mawazo yenu, wala njia zenu si njia zangu; asema BWANA. Kwa maana kama vile mbingu zilivyo juu sana kuliko nchi kadhalika njia zangu zi juu sana kuliko njia zenu, na mawazo yangu kuliko mawazo yenu."*

Tunapoangalia mateso katika mtazamo wa Kimungu, kutoka katika mipango yake kwetu ya kutuandalia umilele, basi tutaanza kushukuru kwa nini ameruhusu mateso kutokea.....

Na usisahau kamwe maneno hayo ya Paulo, ambayo inatukumbusha upendo wa Mungu usiyopungua:

Waru. 8:35-39, *"Ni nani atakayetutenga na upendo wa Kristo? Je ! ni dhiki au shida, au adha, au njaa, au uchi, au hatari, au upanga? Kama ilivyoandikwa ya kwamba, kwa ajili yako tutauawa mchana kutwa,tumehesabiwa kuwa kama kondoo wa kuchinjwa. Lakini katika mambo hayo yote tutashinda, na zaidi ya kushinda kwa yeye aliyetupenda. Kwa maana nimekwisha kujua hakika ya kwamba, wala*

mauti, wala uzima, wala malaika, wala wenye mamlaka, wala yaliopo, wala yatakayokuwapo, wala wenye uwezo, wala yaliyo juu, wala yaliyo chini, wala kiumbe kinginecho chote hakitaweza kututenga na upendo wa Mungu ulio katika Kristo Yesu Bwana wetu."

Mungu na atukuzwe!